Kuzuia Majaribio ya Nyuklia, Kukuza Amani

# Mkataba wa CTBT na Afrika

CTBTO
PREPARATORY COMMISSION

# Wajibu wa Afrika katika Kuzuia Kuongezeka na Uondoaji

## Mkataba wa Kuzuia Kuongezeka kwa Silaha za Nyuklia (NPT)

Mataifa ya Afrika kwa muda mrefu yamekuwa katika mstari wa mbele kwenye juhudi za kimataifa za kufikia lengo la kuzuia kuongezeka na uondoaji wa silaha za nyuklia, hili likichochewa na historia yao kama eneo ambalo majaribio ya nyuklia yaliwahi kufanywa.

Karibia nchi zote katika eneo hilo ni wanachama wa Mkataba wa Kuzuia Kuongezeka kwa Silaha za Nyuklia (NPT).

Mkataba wa NPT unalenga kuzuia kuongezeka kwa silaha za nyuklia na teknolojia ya silaha hizo, kukuza ushirikiano katika matumizi salama ya nishati ya nyuklia na kuendeleza lengo kuu la uondoaji wa silaha za nyuklia. Katika utangulizi wake, kwa kuzingatia lengo la Mkataba wa Kupiga Marufuku Majaribio ya Nyuklia (CTBT), unalenga kufikia lengo la "kusitishwa kabisa kwa majaribio yote ya ulipuzi wa silaha za nyuklia."

### Mkataba wa Pelindaba

Mkataba wa Ukanda Usio na Silaha za Nyuklia wa Afrika, pia unajulikana kama Mkataba wa Pelindaba, unaonyesha zaidi kujitolea kwa Afrika kuhakikisha kuwa wana mustakabali wa kukomesha silaha za nyuklia. Mkataba huu ulitambua bara zima - eneo linalozidi kilomita za mraba milioni 30 km² - kama eneo lisilo na silaha za nyuklia, na kuifanya kuwa eneo kubwa zaidi la aina hiyo ulimwenguni. Ulianza kutumika mwaka wa 2009, kufuatia uidhinishaji wake na nchi 28.

Mkataba wa Pelindaba unapiga marufuku utafiti, uundaji, utengenezaji, uhifadhi, ununuaji, umiliki, udhibiti au uwekaji wa silaha za nyuklia. Mkataba huu pia unazuiamajaribio ya nyuklia, kwa kuzingatia dhamira ya Shirika lililounda Mkataba wa kuzuia Majaribio ya Nyuklia (CTBTO).

### Tume ya Afrika ya Nishati ya Nyuklia (AFCONE)

Ili kusimamia utekelezaji wake, mkataba huo uliunda Tume ya Afrika ya Nishati ya Nyuklia (AFCONE), yenye makao yake makuu Pretoria, Afrika Kusini. AFCONE inahakikisha uzingatiaji wa masharti ya mkataba na kusaidia kuhamasisha matumizi ya amani ya teknolojia ya nyuklia katika bara zima.

**Mkataba wa Pelindaba**



**Mkataba wa Pelindaba** unatambua Afrika kama ukanda usio na silaha za nyuklia. Mkataba huo uliotiwa sahihi mwaka wa 1996 na kuanza kutumika mwaka wa 2009, unapiga marufuku uendelezaji, majaribio, umiliki na uwekaji wa silaha za nyuklia katika bara hili.

Mkataba huo ni hatua muhimu kuelekea kufikia lengo la uondoaji wa silaha za nyuklia duniani na unathibitisha kujitolea kwa eneo kuimarisha amani na usalama.




Cissé Yacouba, Balozi Bora na Mwenye Mamlaka Kamili, Mwenyekiti wa Tume ya Maandalizi ya 2025, kikao cha pamoja cha WGA-WGB




Katibu Mtendaji wa CTBTO Robert Floyd katika Kamati ya Maandalizi ya Mkataba wa NPT, Umoja wa Mataifa, mwaka wa 2022

# Wajibu Wa Afrika kwenye mkataba wa CTBT

Afrika ni mshirika mkuu katika juhudi za kimataifa za kuendeleza malengo ya mkataba wa CTBT.

Kukiwa na mataifa 54 katika eneo hilo, karibu yote yameidhinisha Mkataba huo - ishara ya kujitolea kwa Afrika kuhakikisha kuwa kuna amani na usalama duniani. Katika muongo uliopita, uanachama wa CTBT umeendelea kuongezeka k taratibu. Hasa, katika mwaka wa 2022, mataifa matatu ya Kiafrika yalikuwa miongoni mwa mataifa saba duniani kote yaliyoidhinisha Mkataba huo. Mwaka huo, kanda ya Afrika ya Kati ilifikia ushiriki kamili kupitia uidhinishaji wa Ginekweta na Sao Tome na Principe, huku uidhinishaji wa Gambia ukiashiria ushiriki kamili katika kanda ya Afrika Magharibi. Kanda ya Kusini mwa Afrika tayari ilikuwa na ushiriki kamili.



"Ninatoa wito kwa mataifa yote ambayo hayajatia sahihi au kuidhinisha Mkataba huo kufanya hivyo... hasa yale mataifa ambayo ni sharti yaidhinishe Mkataba huo ili uanze kutumika."

- Marehemu Kofi Annan, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kutoka Ghana

### Mamlaka za Kitaifa: Kuimarisha Utekelezaji wa CTBT

Zaidi ya mataifa 30 ya Afrika yameweka au kuanzisha mamlaka za kitaifa kuhudumu kama wawasiiani kati ya CTBTO na Mataifa mengine Wanachama. Huluki hizi zenye taasisi mbalimbali zimeundwa na wawakilishi kutoka mamlaka mbalimbali za serikali. Katika baadhi ya nchi, mamlaka hizi zina wajibu muhimu katika kutekeleza Mkataba huo katika ngazi ya kitaifa. Katika nchi nyingine, mamlaka hizi zinalenga kujadiliana na kuhamasisha utiaji sahihi wa mikataba ya vituo au kushirikiana na Shirika kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Takwimu (NDC). Katika hali zote, mashirika haya hukuza ushirikiano wa karibu na wajibu wa pamoja kwa dhamira ya CTBTO.




Mwakilishi wa Kudumu wa Ghana katika mwaka 2024, Balozi Matilda Aku Alomatu Osei-Agyeman, akikutana na Katibu Mtendaji wa CTBTO

### Uongozi kutoka Afrika: Kubadilisha Mwelekeo wa CTBTO

Mataifa ya Afrika yanatekeleza wajibu muhimu katika kazi ya Shirika, ambapo wawakilishi kutoka eneo hilo wanashikilia nyadhifa muhimu za uongozi ndani ya CTBTO. Watu mashuhuri ni pamoja na aliyekuwa Katibu Mtendaji Dkt. Lassina Zerbo kutoka Bukinafaso (2013-2021) na Wenyeviti kadhaa wa Tume ya Maandalizi, ambayo ilianzishwa ili kuweka msingi wa utekelezaji wa CTBT.

Ni pamoja na marehemu Jacob (Jackie) S. Selebi kutoka Afrika Kusini (1996) Mwenyekiti wa kwanza kabisa, pamoja na wawakilishi kutoka Aljeria (1999, 2005, na 2020), Kodivaa (2025), Namibia (2010), na Naijeria (2015).

Uongozi wao umesaidia kuchagiza mwelekeo wa CTBTO na kuimarisha ushirikiano wa kikanda.



Aliyekuwa Katibu Mtendaji wa CTBTO, Dkt Lassina Zerbo kutoka Bukinafaso (2013-2021)

### Umoja wa Afrika (AU)

Umoja wa Afrika (AU) umekuwa mtetezi thabiti wa suala la uzuiaji wa kuongezeka na uondoaji wa silaha za nyuklia, ukifanya kazi kwa karibu na CTBTO ili kuendeleza malengo ya pamoja. Kupitia mikutano na ushirikiano wa ngazi za juu, unaojumuisha suala la mashauriano ndani ya mfumo wa Baraza la Amani na Usalama la AU, Umoja wa Afrika umefanya kazi kikamilifu ili kukuza ushirikiano wa kikanda na kuhimiza mataifa kutia saini na kuidhinisha mkataba wa CTBT.

Pamoja na ushirikiano wake na AU na mashirika yake tanzu, CTBTO inashirikiana na mashirika mengine ya kikanda ambayo mipango yao inalingana na dhamira yake. Washirika wakuu ni pamoja na Shirika la Utafiti wa Kijiolojia la Afrika (OAGS) na Tume ya Afrika ya Kuchunguza Mitetemo ya Ardhi (AfSC).

### Kuimarisha Ushirikiano: Warsha ya Kikanda ya CTBTO Iliyofanyika nchini Gambia

Ili kuimarisha ushirikiano wa Afrika na CTBT, Shirika hilo liliandaa warsha ya kikanda nchini Gambia mwaka wa 2024. Kwa kuwaleta pamoja washiriki 27 kutoka nchi 23, hafla hiyo ilikuza mijadala yenye maana kuhusu jukumu la Mkataba katika kuimarisha usalama wa kikanda na kuhakikisha kuwa Nchi Wanachama zote zinanufaika kikamilifu kutokana na ushiriki wao.

Waliohudhuria walitafiti kuhusu mada muhimu, ikiwa ni pamoja na vipengele vya kisheria na kiufundi vya utekelezaji wa Mkataba na uwezo wa Mfumo wa Kimataifa wa Ufuatiliaji (IMS). Vikao pia viliangazia jitihada za kujenga uwezo.

Kuendeleza mafunzo ya awali ya kikanda yaliyofanyika nchini Misri, Kenya, Moroko, Nijeri, Naijeria, Senegali, Afrika Kusini na Tunisia, warsha hiyo iliimarisha uongozi wa Afrika katika kuendeleza malengo ya CTBT.



Wanahabari wa Afrika katika Warsha ya Kikanda kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa wa CTBTO kwa Nchi Wanachama wa Kundi la Afrika, Iliyofanyika nchini Gambia, 2024

# Mfumo wa Kimataifa wa Ufuatiliaji (IMS)

Afrika inatekeleza wajibu muhimu katika mtandao wa uthibitishaji wa CTBT, ambao hufuatilia sayari ili kuhakikisha kuwa hakuna jaribio la nyuklia litakalofanyika bila kutambuliwa.

Mara baada ya kukamilika, kanda itakuwa na vituo 21 vya kufuatilia mitetemo ya ardhi (Seismic), vituo tisa vya kufuatilia mawimbi ya angani ya sauti ya chini (infrasound), vituo saba vya radionuklidi (Radionuclide) na maabara moja ya radionuklidi (Radionuclide). Isitoshe, Afrika Kusini inashirikiana na Ujerumani kusimamia kituo cha ziada cha kufuatilia mitetemo ya ardhi kilichopo Antaktika.

• **Vituo vya kufuatili mitetemo ya ardhi** hufuatilia mitetemo ya ardhi inayosababishwa na majaribio ya nyuklia ya chini ya ardhi au chini ya maji. Kama ilivyo mitetemo ya ardhi, milipuko ya nyuklia chini ya ardhi husababisha mawimbi ya mitetemo ya ardhi mawimbi, ambayo hutambuliwa na vituo vya IMS. Hata hivyo, mawimbi haya yana sifa tofauti zinazoruhusu wataalamu kutofautisha shughuli za asili za mitetemo ya tektoniki na matukio ya milipuko.

• **Vituo vya kufuatilia** mawimbi ya angani ya sauti ya chini hutambua mawimbi ya sauti ya masafa ya chini yanayosafiri kupitia angahewa kutoka kwenye milipuko ya nyuklia inayofanyika kwenye angahewa au ya ardhini. Milipuko hii huzalisha mawimbi ya angani ya sauti ya chini ambayo yanaweza kusafiri umbali mkubwa, yakitoa ushahidi wa jaribio la nyuklia juu ya ardhi.

• **Vituo vya radionuklidi** hufuatilia hewa ili kuchunguza ikiwa ina chembechembe na gesi zinazotoa mionzi zinazotolewa kwenye angahewa kutokana na milipuko ya nyuklia. Chembechembe hizi hutoa ushahidi muhimu unaoweza kutumika kutambua mlipuko wa nyuklia.

• **Maabara za Radionuklidi** hutoa uchanganuzi wa kina wa sampuli za radionuklidi zilizokusanywa na vituo, zikitoa takwimu sahihi ya hali ya juu ili kuthibitisha na kuelewa asili ya mlipuko wa nyuklia.

• **Vituo Vinavyotumia Mawimbi** ya Sauti Kufuatilia shughuli za chini ya maji vinarekodi ishara zinazotambua mabadiliko katika shinikizo la maji linalosababishwa na mawimbi ya sauti, ambayo huenda yakahusiana na mlipuko wa nyuklia wa chini ya maji.

**Mikataba ya Vituo**

Pamoja na juhudi hizi za ufuatiliaji, mataifa ya kikanda kama Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kenya, Mauritania, Namibia, Nijeri, Senegali, Afrika Kusini, Tunisia, Uganda, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zambia yametia saini mikataba ya kujenga vituo na CTBTO. Mikataba hii inashughulikia masuala ya kisiasa, kisheria, kiteknolojia na kiutendaji, huku ikihakikisha utendakazi mzuri wa vituo vya IMS katika eneo hilo.




**MAREJELEO**

- Mpangilio Mkuu wa Zana za Kutambua Mitetemo ya Ardhini (PS)
- Kituo Kikuu chenye Zana Zinazopima Mitetemo ya Ardhini kutoka Pande 3 (PS)
- Kituo Kidogo chenye Zana Zinazopima Mitetemo ya Ardhini kutoka Pande 3 (PS)
- Kituo cha Radionuklidi (RN)
- Kituo cha Radionuklidi chenye Uwezo wa Kufuatilia Gesi Isiyounganika (RN)
- Maabara ya Radionuklidi (RL)
- Kituo cha Kufuatilia Mawimbi ya Angani ya Sauti ya Chini (IS)

**Vituo Vikuu vya Kuchunguza** 7

| Jiji | Nchiy |
|---|---|
| Bangui | Jamhuri ya Afrika ya Kati |
| Dimbokro | Kodivaa |
| Luxor | Misri |
| Kilimambogo | Kenya |
| Torodi | Naija |
| Boshof | Afrika Kusini |
| Kesra | Tunisia |

**Vituo Visaidizi Kuchunguza Mitetemo ya** 14

| | |
|---|---|
| Lobatse | Botswana |
| Barabara ya Arta | Jibuti |
| Kottamya | Misri |
| Furi | Ethiopia |
| Masuku | Gabon |
| Ambohidratompo | Madagaska |
| Kowa | Mali |
| Midelt | Moroko |
| Tsumeb | Namibia |
| Babate | Senegali |
| Sutherland | Afrika Kusini |
| Mbarara | Uganda |
| Lusaka | Zambia |
| Matopos | Zimbabwe |

**Vituo vya Radionuklidi** 7

| | |
|---|---|
| Edea | Kameruni |
| Addis Ababa | Ethiopia |
| Misratah | Libya |
| Nouakchott | Mauritania |
| Agadez | Naija |
| Cape Town | Afrika Kusini |
| Dar es Salaam | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |

**Maabara ya Radionuklidi** 1

| | |
|---|---|
| Pelindaba | Afrika Kusini |

**Vituo vya kufuatilia mawimbi ya angani ya sauti ya chini** 9

| | |
|---|---|
| Cape Verde Islands | Cabo Verde |
| Bangui | Central African Republic |
| Dimbokro | Côte d'Ivoire |
| Djibouti | Djibouti |
| Nairobi | Kenya |
| Moramanga | Madagascar |
| Tsumeb | Namibia |
| Boshof | South Africa |
| Kesra | Tunisia |



Kipimaji cha mitetemo ya ardhi cha zamani kimeondolewa kwenye kisima kilicho katika kituo kidogo cha kufuatilia mitetemo ya ardhi AS97, Babate, Senegali



Ufungaji wa kifaa katika kituo cha radionuklidi RN13, Edea, Kameruni

# Kuwezesha Afrika Kupitia Takwimu: Matumizi ya Kiraia na Kisayansi



Muonekano wa angani wa kituo cha msingi cha mitetemo PS26, Torodi, Niger



Kituo cha msingi cha mitetemo PS39, Boshof, Afrika Kusini



Kijiji karibu na pwani ya Sumatra, Indonesia, katika magofu baada ya tsunami ya Bahari ya Hindi ya mwaka 2004

Mfumo wa Kimataifa wa Ufuatiliaji, sehemu muhimu ya shughuli za kimataifa za CTBTO, hutambua na kurekodi mamia ya matukio kila siku. Matukio haya, yawe yanatokana na sababu za asili au shughuli za binadamu, hutoa takwimu muhimu inayoweza kutumika katika maeneo mengi ya kiraia na kisayansi.

Katika baadhi ya matukio, Tume ya Maandalizi imetoa idhini kwa CTBTO kushirikisha takwimu moja kwa moja na wahusika wa nje kwa madhumuni haya.

### Onyo la Mapema kuhusu Tsunami

Janga la Tsunami iliyosababishwa na tetemeko la ardhi la Sumatra la mwaka wa 2004 ilionyesha hitaji muhimu la kuwa na mifumo ya kuaminika ya kutoa tahadhari ya mapema.

Ili kushughulikia suala hilo, CTBTO ilianza kushirikisha takwimu ya mitetemo ya ardhi na mawimbi ya sauti ya kufuatilia shughuli za chini ya maji na vituo vya kutoa onyo kuhusu tsunami ulimwenguni kote kutumia idhini ya mikataba baina ya nchi mbili.

Ushirikiano huu umeimarisha uwezo wa nchi kutoa onyo kwa wakati ufaao, hivyo basi kusaidia kuokoa maisha na kupunguza hasara za kiuchumi kutokana na majanga kama haya.

Barani Afrika, Madagaska ni miongoni mwa mataifa ambayo yametia saini mkataba ya utoaji wa onyo kuhusu tsunami, inayoonyesha jinsi tawkimu za CTBTO zinavyoweza kutumika kujenga ustahimilivu na kulinda jamii.

### Ufuatiliaji wa Mitetemo na Mitetemeko ya Ardhi

Takwimu ya ufuatiliaji wa mitetemo ya ardhi ina jukumu muhimu katika kutofautisha milipuko ya nyuklia ya chini ya ardhi kutoka kwenye matukio mengi ya mitetemo ya asili na yaliyochochewa na binadamu yanayotokea kila siku, kama vile matetemeko ya ardhi.

Barani Afrika, baadhi ya maeneo  yako hatarini zaidi kukumbwa na matukioya mitetemo ya ardhi. Bonde la ufa la Afrika Mashariki, linalovuka nchi kama Ethiopia, Kenya, na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huwa na matukioya mara kwa mara ya mitetemo ya tektoniki kutokana na mgawanyiko unaoendelea wa Bamba la Afrika kuwa mabamba ya Nubia na Somalia. Kaskazini mwa Afrikai, Aljeria na Moroko zinakabiliwa na hatari za mitetemo ya ardhi kwa sababu ya eneo lao kuwa karibu na mpaka kati ya bamba za Afrika na Eurasia.

# Vituo vya Kitaifa vya Takwimu (NDCs)

Vituo vya Kitaifa vya Takwimu (NDC) ni kiini cha mfumo wa ufuatiliaji wa kimataifa wa CTBT.

Taasisi hizi za kiufundi huzipa serikali maarifa muhimu kuhusu michakato ya uthibitishaji, na kuziwezesha kufanya maamuzi sahihi na kutimiza wajibu wao chini ya Mkataba huo.



**1**

Kituo cha IMS hutuma takwimu kwa takribani muda halisi hadi kwenye Kituo cha Kimataifa cha Takwimu (IDC) kichopo Vienna.



**2**

Takwimu ghafi huchakatwa kwanza kupitia uchanganuzi wa kiotomatiki, kisha kukaguliwa na wataalamu ili kuzalisha bidhaa za IDC, kama vile muhtasari mkuu, orodha za matukio na taarifa.



**3**

Takwimu ghafi ya IMS na bidhaa za IDC hutumwa mara moja kwa NDC kwa ajili ya kufanyiwa tathmini zaidi.



Mafunzo kwa wawakilishi wa CTBTO kwa wafanyakazi wa NDC kufuatia usakinishaji wa CBS kama sehemu ya mpango wa NDCs4All, Algeria, 2025

Ili kusaidia kuanzisha na kudumisha NDC, CTBTO hutoa vifaa, programu na mafunzo, yanayolenga nchi zinazoendelea.

Shukrani kwa juhudi hizi, na mpango wa National Data Centresfor-All (NDCs4All), zaidi ya Nchi Wanachama 35 barani Afrika zimeanzisha NDC zao.

**Baadhi ya matukio Muhimu za Usaidizi wa NDC barani Afrika**

- Warsha ya Kikanda kwa NDC Zinazozungumza Kiarabu – Aljeria, 2024
- Mafunzo ya Kujenga Uwezo wa NDC kwa Ukanda wa Afrika – Kenya, 2024
- Mafunzo ya NDC kwa Lugha ya Kifaransa – Nijeri, 2023
- Warsha ya Kikanda ya Vituo vya kufuatilia mawimbi ya angani ya sauti
ya chini ya NDC za Afrika – Tunisia, 2018
- Warsha ya Kujenga Uwezo wa NDC kuhusu Muda wa Kusafiri wa Kikanda wa Mitetemo ya Ardhi (RSTT) – Namibia, 2017
- Uundaji, Upimaji na Uthibitishaji wa Muda wa Kusafiri kwa Mitetemo ya Ardhi kwa Ukanda (RSTT) wa Afrika – Misri, 2016

# Uungaji mkono wa Afrika kwa Ukaguzi Unaofanyika kwenye Kituo (OSI)

Ukaguzi Unaofanyika sehemu ya tukio (OSI) ni sehemu ya mwisho ya utaratibu wa uthibitishaji wa CTBT.

Mara baada ya Mkataba kuanza kutumika, Nchi Wanachama zitakuwa na uwezo wa kuomba ukaguzi ili kukusanya ushahidi wa moja kwa moja ikiwa mfumo wa kimataifa wa ufuatiliaji utagundua mlipuko wa nyuklia ulioweza kutokea.

CTBTO imeshirikiana kwa karibu na kanda ya Afrika ili kukuza utaalamu wa kiufundi kupitia shughuli mbalimbali za OSI, ambazo ni pamoja na:

## Kozi za Utangulizi za Kikanda za OSI (zinazoandaliwa Afrika zikiwahusisha wataalamu kutoka maeneo mbalimbali ya ukanda huo)

### Kozi ya 21 ya Utangulizi ya Kikanda ya OSI (RIC21) – Afrika Kusini, 2016

Kozi hii ya msingi ilitoa utangulizi wa kanuni za OSI kwa wataalamu kutoka mataifa 33 ya Afrika., ikiwapa maarifa kuhusu dhana kuu, teknolojia, na taratibu za kiutendaji. Iliweka msingi wa ushirikiano wa baadaye katika juhudi za uthibitishaji.

### Kozi ya 26 ya Utangulizi ya Kikanda ya OSI (RIC26) – Misri, 2024

Hii ilikuwa kozi ya pili ya aina yake barani Afrika. RIC26 iliwaleta pamoja wataalamu wa kiufundi kutoka mataifa 26 ya kanda, na kuimarisha utaalamu wa kusaidia juhudi za uthibitishaji za CTBT.



Toleo la 26 la Kozi ya Utangulizi ya Kikanda ya OSI (RIC), Misri, 2024

## Mafunzo ya Wakaguzi Wasaidizi wa OSI (yaliyofanyika Afrika yakihusisha wakaguzi kutoka mataifa mbalimbali duniani)

### Kozi ya Kiwango cha Juu ya OSI – Afrika Kusini, 2018

Washiriki 70 kutoka Nchi Wanachama 44 duniani kote walishiriki katika mpango huu. Ili muundo wa mafunzo uwaandae washiriki kwa shughuli za vitendo vya OSI, kozi ilijumuisha mbinu mbalimbali, ikisisitiza uzoefu wa mafunzo kwa vitendo halisi.

### Kozi ya Utazamaji Kutoka Ardhini na Angani ya OSI – Afrika Kusini, 2018

Ili kuendeleza mafunzo ya Kiwango cha Juu, washiriki 16 wa mafunzo ya wakaguzi wasaidizi kutoka Nchi Wanachama 15 walishiriki katika mafunzo haya.

Mafunzo yalilenga juu ya matumizi ya vifaa kwa ajili ya uchunguzi wa kuona na ufuatiliaji wa maeneo, ikiwa ni pamoja na maandlizi  kabla ya safari ya ndege na helikopta na mazoezi ya vitendo halisi katika kutambua viashiria vinavyohusiana na OSI kwa kutumia mbinu za ardhini na angani.



Kozi ya Kiwango cha Juu ya OSI – Afrika Kusini, 2018

## Ushiriki wa Wataalamu wa Afrika katika Shughuli Nyingine za OSI

### Warsha za OSI

Warsha za OSI zina jukumu muhimu katika kuimarisha kipengele cha OSI cha utaratibu wa uthibitishaji wa CTBT kwa kuzingatia mada maalum kwa vitendo. Kwa kipindi cha miaka mingi, zaidi ya wataalam 50 kutoka nchi za Afrika wamekuwa wakishiriki kikamilifu katika warsha hizi, na kuchangia ujuzi wa kikanda na kimataifa.



Mshiriki kutoka Afrika anayehudhuria warsha ya RIC-26, iliyoandaliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Unajimu na Jiofizikia ya Misri (NRIAG), 2024

### Mazoezi ya OSI

Mazoezi ya OSI yanatoa fursa ya kujaribu na kuthibitisha shughuli za ukaguzi, mbinu, michakato, na taratibu kwa njia jumuishi. Mazoezi haya ni muhimu sana katika kuendeleza kipengele cha OSI cha mfumo wa uthibitishaji. Washiriki wengi ni wakaguzi wasaidizi wa OSI waliopata mafunzo, huku wataalamu kutoka nchi za Afrika wakishiriki mara kwa mara katika mazoezi haya.



Washiriki kutoka Afrika wakati wa Mazoezi ya Mwanzo ya OSI (BUE24), Hungaria, 2024



Mazoezi Lengwa ya OSI (DEs), Austria, 2023

# Kuchagiza Mustakabali: Fursa kwa Vijana na Wanawake

Wafanyakazi wa CTBTO wana uhitimu wa juu sana na wana ujuzi na ustadi wa kipekee. Huku msisitizo mkubwa ukiwa juu ya uanuai na ujumuishaji, Shirika hilo linaongozwa na "G tatu": usawa wakijinsia, kijiografia na kizazi (gender, geographical, and generational ). Kanuni hizi zinahakikisha kuwa michango mikubwa kutoka kwa mitazamo mbalimbali inakuzwa.

Nguzo muhimu ya "G tatu" ni uwakilishi wa kizazi, ambao unatanguliza ushirikishaji na kuwawezesha vijana. Kwa kutoa fursa za elimu, utetezi, na ushirikiano, CTBTO inahamasisha kizazi kijacho kuchangia kikamilifu katika dhamira yake ya kuunda mustakabali ulio salama zaidi.

Ili kusaidia lengo hili, Shirika limezindua mipango kadhaa yenye athari kubwa:

### Kikundi cha Vijana cha CTBTO (CYG)

Likiwa na zaidi ya wanachama 250 kutoka mataifa ya Afrika, kikundi hiki kinahimiza wataalamu wachanga na wanafunzi kuongeza ujuzi wao na kukuza ufahamu kuhusu malengo ya Shirika.

### Mpango wa Unasihi wa CTBTO

Mpango huu unawawezesha wanawake walio katika hatua za mwanzo za kazi katika nyanja za STEM, kwa lengo maalum kwa washiriki kutoka maeneo yasiyo na uwakilishi mkubwa, ikiwa ni pamoja na Afrika. Kwa kukuza uendelezaji wa ujuzi na maendeleo ya kazi, mpango huu unachangia kujenga jamii jumuishi zaidi katika sayansi, teknolojia, uhandisi, na hisabati.

### Mpango wa Utafiti wa Ushirika

Mpango ulioanzishwa kwa ushirikiano na Kituo cha Mafunzo ya Nishati na Usalama (CENESS), mpango huu unahamasisha ushirikiano katika maeneo muhimu ya utafiti na ushiriki mkubwa kutoka kwa wawakilishi wa Afrika umeonekana.

Juhudi hizi kwa pamoja zinahakikisha kwamba viongozi wenye uwezo na waliowezeshwa vizuri kutoka Afrika na sehemu nyingine za dunia wanaunda mustakabali wa usalama wa dunia.



Mshiriki wa Mpango wa Unasihi wa CTBTO katika Kongamano la Diplomasia ya Sayansi ya CTBT, Vienna, 2022



Washiriki wa Vijana katika Kongamano la Diplomasia ya Sayansi la CTBT, Vienna, 2022



Mshiriki wa Mpango wa Unasihi wa CTBTO katika Mkutano wa Sayansi na Teknolojia, Vienna, 2023

CTBTO
PREPARATORY COMMISSION

2025

Sehemu ya Taarifa kwa Umma ya Tume ya Maandalizi ya Shirika la Mkataba wa Kupiga Marufuku Majaribio ya Nyuklia (CTBTO)

Vienna International Centre, P.O. Box 1200, 1400 Vienna, Austria | info@ctbto.org | WWW.CTBTO.ORG

© Tume ya Maandalizi ya CTBTO, Imechapishwa Austria, 2025